**MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 21.10.2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA BUKOBA**

## 1.0 WAJUMBE WALIOHUDHURIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Murshid H. Ngeze | Diwani Kata Rukoma | Mwenyekiti |
| 2. | Bibi Fatina H. Laay | Mkurugenzi Mtendaji | Katibu |
| 3. | Mhe. Privatus A. Mwoleka | Diwani Kata Bujugo | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Nuru Kabendera | Diwani Kata Katerero | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Pastory A. Kabelinde | Diwani Kata Mugajwale | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Jasintha B. Gabriel | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Samwel A. Makwabe | Diwani Kata Karabagaine | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Gideon Banyenza | Diwani Kata Rubafu | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Khatwibu M. Kahyoza | Diwani Kata Kemondo | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Anneth Y. Kajuna | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Restuta K. Mugashe | Diwani Kata Kishanje | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Stanley N. Nestory | Diwani Kata Kaagya | Mjumbe |

## 1.1 WAJUMBE WASIOHUDHURIA

1. Mhe. Dkt. Jasson S. Rweikiza — Mbunge wa Bukoba Vijijini - Kwa taarifa

## 1.2 WATENDAJI WALIOHUDHURIA.

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Dotto O. Stambuli | Kaimu Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi. |
| 2. | Bw. Abubakari Baelejanya | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 3. | Dkt. Kisanga Makigo | Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi |
| 4. | Bw. Babylus Mashauri | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika |
| 5. | Bw. Albert Msemo | Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji |
| 6. | Dr. Bandioti Gavyole | Mkuu wa Idara ya Afya |
| 7. | Bw. Faraja Maduhu | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 8. | Bibi. Consolatha Joseph | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 9. | Bw. Thobias Shija | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 10. | Bw.Solomon Mwangosi | Mkuu wa Kitengo cha Ugavi |
| 11. | Bw. Joseph Matope | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 12. | Bw. Dominick Rutatinisibwa | Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira |
| 13. | Bibi. Getrude Mathia | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Nyuki |
| 14. | Bibi. Patricia Minja | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. |
| 15. | Bw. Emmanuel Chinduwoli | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi |
| 16. | Adv. Daniel Mbaki | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria |
| 17. | Bw. Eradius Mukebezi | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |
| 18. | Bw. Robert Kapufi | Afisa Tarafa Kyamtwara |
| 19. | Bw. Edwin Kyebishanda | Afisa Tarafa Rubale |



Scanned with CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| 20. | Bw. Lastus Zahabu | Afisa Tarafa Bugabo |
| 21. | Bw. Erasto M. Iluganyuma | Afisa Tarafa Katerero |
| 22. | Bibi. Paschazia Paul | Mwandishi wa Vikao |
| 23. | Bw. Erasmus Evarister | Mwandishi wa Vikao |

## 2.0 MUHT.NA.115/2019: KUFUNGUA KIKAO

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afungue kikao baada ya akidi kutimia.

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao na kueleza kuwa kikao hiki ni maalum kwa ajili ya kujadili taarifa ya mapokezi ya Shilingi 1,700,000,000/=kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 85 katika shule za sekondari zilizopokelewa kupitia fedha za uviko – 19.

Aliwataka wajumbe wawe makini katika kujadili agenda zote zilizokuwa mbele yao.

Mwenyekiti alifungua kikao saa 07:08 Mchana.

## 3.0 MUHT.NA.116/2019: AGENDA ZA KIKAO

Agenda za kikao hicho zilikuwa kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kikao.

2. Maombi ya matumizi ya fedha za UVIKO 19 kiasi cha Tshs. 1,833,405,822.51

3. Kuteuwa wajumbe wa Kamati ya uratibu na ufuatilaiji wa ujenzi wa vyumba vya madarasa 85 kupitia mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO – 19 kwa kutumia fedha za Shirika la Fedha Duniani.

4. 4.Kufunga Kikao

## 4.0 MUHT.NA.117/2021 MAOMBI YA MATUMIZI YA FEDHA ZA UVIKO 19 KIASI CHA TSHS. 1,833,405,822.51

Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha maombi ya matumizi ya fedha za UVIKO 19 kiasi cha Tshs. 1,833,405,822.51 akieleza kuwa Halmashauri ya Wilaya Bukoba imepokea jumla ya Tshs. **1,833,405,822.51** kutoka IMF mnamo mwezi Oktoba, 2021. Fedha hizi ni kwa ajili ya Program maalum ya UVIKO 19 ikiwa ni utekelezaji wa miradi kama ifuatavyo:-

i) Ujenzi wa madarasa 85 kwa Shule za Sekondari kwa gharama ya Tshs. 1,700,000,000/=
ii) Ujenzi wa nyumba 1 ya watumishi (Three in One) yenye thamani ya Tshs. 90,000,000/=



Scanned with CamScanner

Aidha sehemu ya fedha hizi ni kwa ajili ya hamasa ya chanjo ya UVIKO 19 Tshs. 36,891,075.51 na gharama za ufuatiliaji na tathimini Tshs. 6,514,747.

Miradi hii itatekelezwa kwa force akaunti ili kupunguza gharama na kukamilisha miradi kwa wakati.

Kikao kilipokea taarifa kwa mjadala:-

Mjumbe alitoa shukrani za dhati kwa Serikali kwa kuleta fedha hizo na kusema kuwa itasaidia kupunguza kero ya uhaba wa vyumba vya madarasa na hivyo kuondoa mlundikano wa wanafunzi katika madarasa.

Mjumbe alishauri kuwa wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo Halmashauri ihakikishe inasimamia kwa karibu ujenzi huo ili miradi itekelezwe kwa kiwango stahiki na kukamilika kwa wakati.

Baada ya mjadala kikao kilikubaliana na maombi hayo kisha kuagiza kuwa taratibu ziendelee.

## 6.0 MUHT.NA.118/2021 KUFUNGA KIKAO

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge kikao baada ya agenda zote kujadiliwa na kukamilika.

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa namna walivyojadili agenda zote kikamilifu. Alitaka pindi ujenzi wa miradi hiyo utakapoanza Halmashauri isimamie kikamilifu kuhakikisha kuwa inatekelezwa ipasavyo na thamani ya fedha inaonekana.

Alifunga kikao saa 08:05 mchana.

MWENYEKITI.................. UMETHIBITISHWA NA;

KATIBU..................

TAREHE

.........21/10/2021.................................



Scanned with CamScanner